Ibrahimu, Rafiki wa Mungu

na

Ellis Forsman

Ibrahimu, Rafiki wa Mungu

na

Ellis Forsman

Oktoba 8, 2011

Ibrahimu, Rafiki wa Mungu

Yakobo 2:23

Yakobo, kwa kuwaambia umuhimu wa "kufanya" vile vile "kuamini", anamuonyesha Ibrahimu kama rafiki wa Mungu.

Yak. 2:23. "*Maandiko yale yakatimia yaliyonena, Ibrahimu ali mwamini Mungu ikahesabiwa kwake kuwa ni haki; naye aliitwa rafiki wa Mungu."*

Hii ili elezwa mara mbili katika Agano la Kale.

- 2 Nyakati 20:7, *"Si wewe, Ee Mungu wetu, uliye wafukuza wenyeji wan chi hii mbele ya watu wako Israeli, ukawapa wazao wa Ibrahimu rafiki yako hata milele?"*
- Isa. 41:8, *"Nawe Israeli mtumishi wangu; Yakobo, niliyekuchagua; mzao wa Ibrahimu rafiki yangu."*

Musa ndiye mtu pekee aliyechaguliwa kama wengine katika Biblia. Hakika, akiwa ameonyeshwa hivyo, mtu huyu anafaa kujifunza kwake.

Mungu alimchagua Ibrahimu kuwa mtu ambaye kupitia yeye tunabarikiwa

Mwanzo 12:1-4, *"BWANA akamwambia Abramu, Toka wewe katika nchi yako na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha; name nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki na kulikuza jina lako nawe uwe Baraka, name nita wabariki wakubarikio, naye akulaaniye nita mlaani, na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa. Basi, Abram akaenda kama BWANA alivyomwamuru; Lutu akaenda pamoja naye. Naye Abram alikuwa mtu wa miaka sabini na mitano alipotoka Harani."*

Anasemwa kuwa ni baba wa wote wanaoamini.

Warumi 4:11, *"Naye aliipokea dalili hii ya kutahiriwa, muhuri wa ile haki ya imani aliyokuwa nayo kabla hajatahiriwa; apate kuwa baba yao wote waaminio, ijapokuwa hawakutahiriwa, ili na wao pia wahesabiwe haki."*

Huyu aliye na uhusiano wa karibu na waaminio, alikuwa ni rafiki wa Mungu. Hakika, tunahitaji kujua zaidi kuhusiana na mtu huyu aliyeitwa rafiki wa Mungu.

Ibrahimu alikuwa na Imani kuu

- Yako. 2:21-23, *"Je! Baba yetu Ibrahimu hakuhesabiwa kuwa na haki kwa matendo, hapo alipomtoa Isaka mwanawe juu ya madhabahu? Waona kwamba imani ilitenda kazi pamoja na matendo yake. Maandiko yale yakatimizwa yaliyonena, Ibrahimu alimwamini Mungu; ikahesabiwa kwake kuwa ni haki, naye aliitwa rafiki wa Mungu."*
- Mwanz. 15:6, *"Na alimwamini BWANA; akahesabiwa haki."*

Kuwa na imani kuu inawafanya wanadamu wapendeze machoni pa Mungu.

Waeb. 11:6, *"Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao."*

Kuna watu katika Biblia wasiyohesabika ambao wameonyesha imani yao kwa Mungu. Hiki ni kitu ambacho wote tuna nafasi ya kukifanya ili kumpendeza. Mara nyingi, watu husema wanamwamini Mungu, lakini siyo zaidi sana kufuata kile anachokisema.

Miaka kadhaa iliyopita, nilikuwa naongea na mfanyakazi mwenzangu kuhusu kuwa mkristo. Alionekana kukubaliana na kila kitu nilichomwambia. Hatimae, akasema, "najua Biblia inasema lazima nibatizwe, lakini nafikiria atanisamehe katika swala hili, kwa sababu ninaogopa maji." Nimesikia watu wakiambia wenzao hivyo Mungu ameufungua mlango kwa ajili yao, na kwa wengine ambao kwa sababu Fulani wanaingia katika njia hiyo, dirisha limefunguliwa kwa wengine. Watu wanatoa wapi maneno ya upuuzi. Hakika haitoki katika Biblia. Tukijaribu kuingia katika njia nyingine, anatuchukulia kama wezi na majambazi.

Ibrahimu alikuwa mtiifu

- Waeb. 11:8, *"Kwa imani Ibrahimu alipoitwa aliitika, atoke aende mahali pale atakapopapata kuwa urithi; akatoka asijue aendako."*
- Waeb. 11:17, *"Kwa imani Ibrahimu alipojaribiwa, akamtoa Isaka awe dhabihu; nay eye aliyezipokea hizo ahadi alikuwa akimtoa mwanawe, mzaliwa pekee."*

Nuhu alionyesha uaminifu uliyo kamili kwa Mungu kwa kuijenga safina kwa ajili ya mafuriko, wakati ambapo ilikuwa haijanyesha hapo nyuma mvua kubwa. Nchi ili jaa umande, na siyo mvua. Ibrahimu

akaonyesha uaminifu mkuu kwa Mungu kwa kwenda sehemu ambapo hakupajua. Hakusita; aliamka mara moja Mungu alipomuita.

Ibrahimu akaonyesha uaminifu mkuu kwa Mungu na utii alipoambiwa kumtoa sadaka motto wake mwenyewe, Isaka, katika madhabahu.

Mwanzo 22:9-12, *"Wakafika mahali pale alipoambiwa na Mungu, Ibrahimu akajenga madhabahu huko, akaziweka tayari kuni, kasha akamfunga Isaka mwanawe, akamweka juu ya madhabahu, juu ya zile kuni. Ibrahimu akanyosha mkono wake akakitwaa kisu ili amchinje mwanawe. Ndipo malaika wa BWANA akamwita kutoka mbinguni, akasema, Ibrahimu! Ibrahimu! Naye akasema mimi hapa. Akasema usimnyoshee kijana mkono wako, wala usimtendee neno, kwa maana sasa ninajua ya kuwa unamcha Mungu, iwapo hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee."*

Huo ni wingi wa uaminifu na utii. Watu wengi katika dini mbali mbali za ulimwengu hawawezi kwenda jinsi Ibrahimu alivyofanya.

Lazima tumtii ndipo tumpendeze

Math. 7:21,*"Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni."*

Zingatia Yakobo 1:21-25,*"Kwa hiyo wekeeni mbali uchafu wote na ubaya uzidio, na kupokea kwa upole neno lile lililopandwa pandwa ndani liwezalo kuziokoa roho zenu. Lakini iweni watendaji wa neno wala si wasikiaji tu,hali mkijidanganya nafsi zenu. Kwa sababu mtu akiwa ni msikiaji wa neno tu, wala si mtendaji, mtu huyo ni kama mtu anayejiangalia uso wake katika kioo. Maana hujiangalia kasha huenda zake, mara akasahau jinsi alivyo. Lakini aliyeitazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru na kuka humo, asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika utendaji wake."*

Ibrahimu alimwogopa Mungu

Mwanzo 22:12, *"Akasema usimnyoshee kijana mkono wako wala usimtende neno; kwa maana sasa ninajua ya kuwa unamcha Mungu, iwapohukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee."*

Umewahi kusikia watu wanasema wanachagua kumpenda Mungu, na si kumwogopa. Hiki ni kitu ambacho Mungu hajaamuru. Bali aliamuru vyote.

- Kumbukumbu 6:1-2, *"Na hii ndiyo sheria, na amri, na hukumu, alizoziamuru Bwana Mungu wenu, mfundishwe mpate kuzitenda*

katika inch ile mnayoivukia kuimiliki; upate kumcha Bwana Mungu wako, kushika amri zake zote na sheria zake, ninazakuamuru wewe, na mwanao, na mwana wa mwanao, siku zote za maisha yako, tena siku zako ziongezwe."

- Mhubiri 12:13, *"Hii ndiyo jumla ya maneno yote, yamekwisha sikiwa; mche Mungu, nawe uzishike amri zake, maana kwa jumla ndiyo impasavyo mtu."*

Ndiyo, tunapaswa kumpenda Mungu, lakini pia tuwe na uoga uliowazi kwake yeye, kama motto anavyojifunza kutii kutoka kwa baba. Kila mzazi anatakiwa ajue wazo hili. Nabii anasema kwa ujumla ndiyo ipasavyo mtu.

Ibrahimu alikuwa na upende na wengi

Mwanzo 18:23-32, *"Ibrahimu akakaribia akasema, je! Utaharibu mwenye haki pamoja na mwovu? Huenda wakawepo wenye haki hamsini katika mji, utaharibu wala hautauacha mji kwa ajili ya hao hamsini wenye haki waliomo? Hasha usifanye hivyo, ukamwue mwenye haki pamoja na mwovu, mwenye haki awe kama mwovu. Hash; mhukumu ulimwengu wote asitende haki? BWANA akasema nikiona katika Sodoma wenye haki hamsini mjini nitapaacha mahali pote kwa ajili yao. Ibrahimu akajibu akasema basi nimeshika kusema na Bwana nami ni mavumbi na majivu tu. Huenda wakapunguka watano katika wale hamsini wenye haki je! Utaharibu mji wote kwa kupungua watano? Akasema sitahuaribu, nikiona humo arobaini na watano. Akazidi tena kusema naye, akinena, huenda wakaonekana na humo arobaini? Akasema, sitafanya kwa ajili ya hao arobaini. Akasema Bwana asiwe na hasira, name nitasema huenda wakaonekana huko thelathini. Akasema sitafanya nikiona humo thelathini. Akasema tazama nimeshika kusema na Bwana huenda wakaonekana huko ishirini? Akasema, sitaharibu kwa ajili ya hao ishirini. Akasema, Bwana asiwe na hasira name nitasema mara hii tu, huenda wakaonekana huko kumi? Akasema sitaharibu kwa ajili ya hao kumi.*

Mungu pia alikuwa na upendo huo

Yoh. 3:16, "*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanaye wa pekee, ilikila amwamiye asipotee bali awe na uzima wa milele."*

Paulo naye akawa na upendo huo

- Rumi. 1:14-16, *"Nawiwa na Wayunani na wasio Wayunani, nawiwa na wenye hekima na wasio na hekima, kwa hiyo kwa*

upande wangu mimi ni tayari kuihubiri injili hata na kwenu ninyi mnaokaa Rumi. Kwa maana siionei haya injili, kwa sababu ni uwezo wa Mungu uletao wokovu kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza na kwa Myunani pia."

- Rumi 10:1-3, *"Ndugu zangu nitakayo sana, moyoni mwangu, na dua yangu nimwombayo Mungu, ni kwa ajili yao ili waokolewe. Kwa maana nawashuhudia kwamba wana juhudi kwa ajili ya Mungu, lakini si hakika maarifa. Kwa maana wakati hawaijui haki ya Mungu, na wakitaka kuithibitisha haki yao wenyewe, hawakujitia chini ya haki ya Mungu."*

Je tuna upendo kama huo kwa wengine?

- Wafil. 2:4, *"Kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo yaw engine."*
- Math. 9:36-38, *"Na alipowaona makutano aliwahurumia, kwa sababu walikuwa wamechoka na kutawanyika kama kondoo wasio na mchungaji. Ndipo alipowaambia wanafunzi wake, mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache. Basi mwombeni Bwana wa mavuno, apelike watenda kazi katika mavuno yake."*

Je tuna upendo kama huu dhidi yaw engine? Si tu kuwajali katika mahitaji yao ya kimwili, bali pia mahitaji yao ya kiroho pia.

Ibrahimu aliheshimu kitengo cha Mungu

Mwanzo 18:19, *"Kwa maana nimemjua ya kwamba atawaamuru wanawe, na nyumba yake baada yake waishike njia ya BWANA, wafanye haki na hukumu, ili kwamba BWANA naye akamtimizie Ibrahimu ahadi zake."*

Tunapaswa kuwa na heshima kuu dhidi ya kitengo cha Mungu, pia. Hii inajumlisha nyumbani, kanisani, hata pia serikali.

Waef. 6:1-9, *"Enyi watoto watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki. Waheshimu baba yako na mama yako; amri hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi, upate heri ukae siku nyingi katika dunia, nanyi akina baba msiwachokoze watoto wenu; bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana. Enyi watumwa, watiini wao walio bwana zenu kwa jinsi ya mwili, kwa hofu na kutetemeka, kwa unyofu wa moyo, kana kwamba ni kumtii Kristo; wala si kwa utumwa wa macho tu kama wajipendekezao kwa wanadamu, bali kama watumwa wa Kristo, mkitenda yampendezayo Mungu kwa moyo. Kwa nia njema kama kumtumikia Bwana wala si wanadamu; mkijua ya kuwa kila neno jema*

alitendalo mtu atapewa lilo hilo na Bwana kwamba ni mtumwa au kwamba ni huru. Nanyi akina bwana, watendeeni wao yayo hayo mkiacha kuwaogofya, huku mkijua ya kuwa yeye aliye Bwana wao na wenu yuko mbinguni, wala kwake hakuna upendeleo."

Kanisa linaitwa bibi harusi wa Kristo. Kama bibi harusi anavyo mtii mmewe, kadhalika na kanisa nalo.

Kumbuka, wawili wanapoana, mke anatumia jina la mume. Hata kama wameoana karibuni, hii ilikuwepo toka mwanzo.

Mwanz.5:2, "*Mwanamume na mwanamke aliwaumba, akawabariki akawaita jina lao Adamu, siku ile walipoumbwa.*"

Wengine wanafikiria kuwa wanaweza kumheshimu Mungu, lakini sio serikali ya wanadamu.

Waru.13:1-6, *"Kila mtu na aitii mamlaka iliyo kuu; kwa maana hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu; na ile iliyopo umeamuriwa na Mungu. Hivyo amwasiye mwenye mamlaka hushindana na agizo la Mungu, nao washindanao watajipatia hukumu. Kwa sababu watawalao hawatishi watu kwa sababu ya matendo mema, bali kwa sababu ya matendo mabaya. Basi wataka usimwogope mwenye mamlaka? Fanya mema, nawe utapata sifa kwake; kwa kuwa yeye ni mtumishi wa Mungu kwako kwa ajili ya wema. Lakini ufanyapo mabaya,ogopa kwa maana hauchukui upanga bure kwa kuwa ni mtumishi wa Mungu, amlipizae kisasi mtenda mabaya kwa ajili ya ghadhabu tu. Kwa hiyo ni lazima kutii si kwa sababu ya ile ghadhabu tu ila na kwa sababu ya dhamiri. Kwa sababu hiyo tena mwalipa kodi, kwa kuwa wao ni wahudumu wa Mungu, wakihudumu katika kazi iyo hiyo."*

Tito 3:1, *"Uwakumbushe watu kunyenyekea kwa wenye uwezo na mamlaka, na kutii, na kuwa tayari kwa kila kazi njema."*

Ibrahimu hakuwa mbinafsi

Mwanzo 13:1-12,*Abramu akapanda kutoka Misri, yeye na mkewe na kila alichokuwa nacho, na Lutu pamoja naye mpaka kusini. Naye Abramu alikuwa ni tajiri sana kwa mifugo, kwa fedha, na kwa dhahabu. Akaendelea kusafiri kutoka kusini mpaka Betheli, mahali pale palipokuwapo hema yake kwanza kati ya Betheli na Ai; napo ndipo palipokuwa na dhahabu aliyofanya hapo kwanza; naye Abramu akalitia jina la BWANA hapo. Na Lutu aliyesafiri pamoja na Abaramu, yeye naye alikuwa na makundi ya ng'ombe na kondoo, na hema. Na ile nchi haikuwatosha, ili wae pamoja, maana mali zao zilikuwa nyingi, hatawasiweze kukaa pamoja. Kukawako ugomvi kati ya wachunga wanyama wa Abramu, na wachunga wanyama wa Lutu; na siku zile*

Wakaanani na Waperizi walikuwa wakikaa katika nchi. Abramu akamwambia Lutu, basi usiwepo ugomvi, nakusihi kati ya mimi na wewe, wala kati ya wachungaji wangu na wachungaji wako; maana sisi tu ndugu. Je! Nchi hii yote haiku mbele yako? Basi ujitenge nami, nakusihi, ukienda upande kushoto, nitakwenda upande wa kuume, ukienda upande wa kuume nitakwenda upande wa kushoto. Lutu akainua macho yake, akaliona Bonde lote la Yordani, ya kwamba lote pia lina maji, kabla BWANA hajaharibu Sodoma na Gomora lili kuwa kama bustani ya Bwana,m kama nchi ya Misri hapo unapokwenda Soari. Basi Lutu akajichagulia bonde lote la Yordani, Lutu akasafiri kwenda upande wa mashariki; wakatengana wao kwa wao. Abramu akakaa katika nchi ya Kanaani, na Lutu akakaa katika miji ya lile bonde; akajongeza hema yake mpaka Sodoma."

Mkristo lazima ajali na ashirikiane kama anataka kuwa rafiki wa Mungu.

Yako.1:27, *"Dini iliyosafi, isiyo na taka mbele za Mungu baba ni hii kwenda kuwa tazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa."*

Tunaambiwa jinsi tunavyoweza kuwa Marafiki wa Mungu

Yoh. 15:14, *"Ninyi ni marafiki zangu, mkifanya ninayowaamuru."*

Je umeshaanza urafiki huu? Je unaweza kutarajia kuitwa rafiki yake kwa ufupi ukimtii?

Utakuwa na tatizo la kufanya haki. Utatenda dhambi. Mungu atakusamehe kama mtoto anayepotea ukitimiza masharti.

- Matend. 8:22, "Basi tubia uovu wako huu, ukamwombe Bwana ili kama yamkini usamehewe fikira hii ya moyo wako."
- 1 Yoh. 1:8-10, *"Tukusema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe wala kweli haimo mwetu. Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote. Tukisema kwamba hatukutenda dhambi,twamfanya yeye kuwa mwongo wala neno lake halimo mwetu."*

Hitimisho

Kama hujawahi kutii injili kwa kuwa Mkristo, kuna mwaliko unatolewa kwa ajili yako ili uwe rafiki wa Mungu.

Imani. Waeb. 11:6, *"Lakini pasipo imani haiwezekani kumpndeza, kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa dhawabu wale wamtafutao."*

Toba.

- Luka 13:3, *"Nawaambia sivyo, lakini msipotubu ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo."*
- Matend. 17:30, *"Basi zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni, bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu."*

Kiri.

- Waru. 10:9, *"Wala tusimjaribu Bwana, kama wengine wao walivyomjaribu, wakaharibiwa na nyoka."*
- Matend.8:37, *"Filipo akasema, ukiamini kwa moyo wako wote inawezekana, akajibu akasema naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye mwana wa Mungu."*

Ubatizo.

- Marko 16:16, *"Aaminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini atahukumiwa."*
- Matend. 2:38, *"Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."*
- 1 Petr. 3: 21, *"Mfano wa mambo hayo ni ubatizo unaowaokoa ninyi pia sikuhizi; (siyo kuwekea mbali uchafu wa mwili bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu), kwa kufufuka kwake Yesu Kristo."*
- Matend. 22:16, *"Sasa unakaawilia nini? Simama, ubatizwe, uoshwe dhambi zako, huku ukiliitia jina la Bwana."*